## Maswali

1. Mbona Sulemani aliita watu wote pamoja huko Gibeoni?
2. Mungu aliambia Sulemani nini kwa ndoto?
3. Sulemani aliomba nini?
4. Mbona Sulemani aliomba hekima?
5. Mbona Mungu alifurahia Sulemani?
6. Mungu alimpa Sulemani nini tena?
7. Sulemani alifanya mambo gani ya ajabu tena ya hekima?
8. Sulemani alijengea Mungu nini huko Yerusalemu?
9. Hekalu ilijengwa kwa muda gani?
10. Mungu alionyesha namna gani kwamba alikuwa amefurahia

## Majibu

1. Kutoa sadaka na kuwa na karamu ya shukrani.
2. "Niombe chochote utakachotaka."
3. Sulemani aliomba hekima.
4. Alitaka kutawala watu wa Mungu kwa hekima.
5. Mungu alifurahi kwa sababu Sulemani alijali watu wake kuliko yeye mwenyewe.
6. Mungu alimpa Sulemani mali, heshima na maisha marefu.
7. Alijenga majengo mazuri, maboma; aliandika methali na nyimbo; alikuwa na ufahamu wa ajabu kwa mambo mengi.
8. Sulemani alijenga Hekalu.
9. Hekalu ilijengwa kwa miaka 7
10. Utukufu wa Mungu ulijaa Hekaluni.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2 Mwaka wa 2

# 66 Sulemani anachagua hekima

### Kwa Biblia

1 Wafalme 2:1—4 na 1 Wafalme 3:4—15

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alifurahi kwa sababu Sulemani alichagua hekima. Mungu anafurahi wakati tunajali wenzetu na kuwasaidia


### Somo

Sulemani alikuwa kijana mdogo alipotiwa mafuta kuwa Mfalme. Labda alikuwa wa umri wa miaka 20. Alitawazwa kuwa Mfalme wa taifa kubwa mno. Mfalme Daudi alipigana vita na adui wa Israeli wengi. Mfalme Daudi alifanya taifa la Israeli kuwa kubwa sana. Wakati Sulemani alitawazwa kama Mfalme, alitawala eneo kubwa mno.

Daudi alikuwa mtu wa Mungu. Kabla afe, aliambia Sulemani kutembea kwa njia za Mungu. Sulemani alikumbuka hayo mausia mazuri. Alitaka aongoze watu wake kwa kumpenda Mungu na wamwabudu. Sulemani aliita pamoja makuhani wote na watu kwa karamu ya shukrani.




**Israeli wakati wa enzi ya Sulemani**
**Yerusalemu** – Mji mkuu wa Sulemani
**Gibeoni** – Hapa Sulemani alikuwa na ndoto na akachagua hekima
**Ezion-Geberi**– Manowari wa Sulemani walifanya biashara wakisafiri kutoka kwa hii bandari.



Masikani iliyotengenezwa na Musa huko jangwani ilikuwa Gibeoni. Sulemani alileta watu wote Gibeoni ili waabudu Mungu. Sulemani alitolea Mungu sadaka elfu moja za kuteketezwa kwa hiyo madhabahu ya shaba. Sulemani alishukuru Mungu kwa kumfanya Mfalme wa hilo taifa kubwa. Alishukuru Mungu kwa sababu kulikuwa na amani kutoka kwa maadui wao.

Mungu alifurahi kwa sababu Sulemani alimpenda. Mungu alifurahi kwa sababu Sulemani alitaka watu wote wampende na kumwabudu. Usiku huo Mungu alizungumza na Sulemani kwa ndoto. Alimwambia, “Niombe chochote utakacho nikupe.”

Sulemani alijua kwamba yeye bado mdogo sana kutawala taifa la Israeli lilokuwa kubwa. Hakuwa na ujuzi wowote. Israeli lilikuwa taifa liliyochaguliwa na Mungu. Sulemani alikuwa anatawalia Mungu taifa la kipekee sana.

Mfalme alikuwa akiketi kwa lango la mji kila asubuhi. Watu walimkujia Mfalme kutoka kila upande wa nchi. Mfalme angechunguza na kuamua shida na ugomvi wao. Angeamua kesi zilizokuwa ngumu sana. Sulemani alijiona kwamba hana hekima ya kutawala hawa watu.


Sulemani alikumbuka vile Mungu alikuwa mzuri kwa baba yake Daudi. Mungu alikuwa amesaidia baba yake kutawala na hekima. Sulemani aliamua kuomba Mungu ampe hekima. Alitaka hekima ili atawale watu wa Mungu vizuzi

Mungu alifurahi sana kwa sababu Sulemani aliomba hekima. Sulemani hakujitakia chochote. Sulemani alifikiri juu ya watu wake. Aliomba hekima ili awatawale vizuzi. Alitaka kusaidia watu wapende na kumtii Mungu. Mungu alifurahia Sulemani sana.

Mungu alipea Sulemani hekima. Mungu alimpa Sulemani hata na vitu vingine vyenye hakuwa ameomba. Mungu alimpa Sulemani mali, heshima na maisha marefu.

Mungu alifanya Mfalme Sulemani awe na hekima kuu. Sulemani alifanya Ufalme wa Israeli kuwa wa nguvu. Alijenga maboma ya miji na nyumba za maghala. Alijenga nyumba za kawaida na za kifalme nyingi tena nzuri. Sulemani alijenga meli nyingi za kibiashara. Hizi meli zilitoka Ezion-Geberi. Walifanya biashara na nchi za mbali. Hizi meli zililetea Sulemani mali mkubwa nyingi.

Sulemani alinena methali elfu tatu. Aliandika nyimbo elfu moja na mia tano. Sulemani alikuwa na ufahamu wa ajabu, wa wanyama na mimea. Alikuwa na ufahamu mkuu wa masomo tena alikuwa na hekima sana. Wafalme na malkia kutoka ulimwengu mzima walikuja kusikia hekima za Sulemani.



Daudi alikuwa na mpango wa kujenga Hekalu Yerusalemu. Daudi alitaka kujengea Mungu Hekalu. Lakini Mungu akamwambia kwamba mwanawe atajenga Hekalu. Daudi alikusanya dhahabu na fedha nyingi ili ijenge Hekalu nzuri. Kabla afe, aliambia Sulemani ajengee Mungu Hekalu.

Sulemani alijenga Hekalu Yerusalemu. Hekalu ilijengwa sawasawa na vile Mungu aliamrisha. Ramani ya Hekalu ilikuwa sasawa na Maskani. Lakini kwa kipimo ilikuwa mara mbili zaidi. Hekalu hii ilikuwa nyumba ya kifahari. Sulemani alifanyia Mungu Hekalu nzuri sana. Ilijengwa na mawe meupe. Ndani ilitengenezwa na miti ya mierezi kutoka Lebanoni. Huko ndani kwote kulifunikwa kwa dhahabu. Hiyo Hekalu ilijengwa kwa miaka saba. Ilikuwa moja ya nyumba za ajabu ulimwenguni kote. Hekalu hiyo ilisimama kwa miaka 400.

Mwishowe Hekalu ilimalizika.  Sulemani aliita watu wote waje kutoa sadaka. Watu wote walikuja kuabudu Mungu ndani ya Hekalu mpya. Sanduku la Mungu liliwekwa ndani ya Patakatifu Pa Patakatifu. Mungu alifurahia Hekalu yenye Sulemani alijenga. Utukufu wa Mumgu ulijaa ndani ya Hekalu.